# Bilioni 50/- kujenga bandari ya uvuvi Kilwa

Na Mwandishi Maalumu, Kilwa

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Sita imetenga Sh bilioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi wilayani Kilwa katika Mkoa wa Lindi.

Majaliwa alisema bandari hiyo itaongeza kasi ya uvuvi wa kisasa na biashara ya samaki ili kuongeza Pato la Taifa na kuboresha maisha ya wananchi.

Alisema hayo jana alipozungumza na watumishi, madiwani na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Majaliwa alisema mradi huo unatarajia kuchangia ukuaji wa maendeleo kwa wananchi wa Wilaya ya Kilwa na Watanzania kwa ujumla, hivyo akahimiza wananchi wachangamkie fursa hiyo kwa kujenga nyumba za kulala wageni na migahawa kwa kuwa watu wengi watahitaji makazi.

"Wataalamu walishapita katika maeneo yote ya pwani kuanzia pwani ya kutoka Tanga hadi Mtwara na kuridhia kwamba Kilwa ni mahali sahihi kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo kwani eneo la uwanda wake ni zuri na lina kina kirefu ambacho hakihitaji kuongezwa na Mheshimiwa Rais ameridhia ijengwe," alisema Majaliwa.

Wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa waliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuamua kujenga bandari hiyo kwa kuwa itaimarisha biashara ya samaki na kuongeza ajira.

Wakati huohuo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya Sh bilioni 16 kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya elimu mkoani Lindi.

Alisema hayo juzi alipozungumza na wananchi, madiwani na wananchi wa Halmashauri ya Mtama mkoani Lindi.

Majaliwa alitoa mwito kwa watumishi kwenye mkoa huo wahakikishe fedha hizo zinatumika katika kazi iliyokusudiwa na atayezitamani zitamuunguza. Alisema watumishi hao wana wajibu wa kuwatumikia Wana-Mtama na kwamba serikali inataka kuona mabadiliko ya kiutendaji katika maeneo yao.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiangalia michoro ya ujenzi wa mradi wa maji wa Mitwero, Mkwaya na Kitunda wilayani Lindi alipokuwa kwenye ziara ya kikazi mkoani humo juzi. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

## Dk Mpango akemea makundi, migogoro CCM

Na John Gagarini, Kibaha

MAKAMU wa Rais, Dk Philip Mpango ameagiza wanachama na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani wajiepushe na makundi na migogoro ndani ya chama.

Alisema hayo mjini Kibaha alipozungumza na viongozi na wajumbe wa kamati ya utekelezaji ya mkoa. Dk Mpango ni Mlezi wa CCM Mkoa wa Pwani.

Alisema makundi na watu wanaogombana ndani ya chama kabla na baada ya uchaguzi ni adui na saratani inayotakiwa kutibiwa mapema

"Tuepuke siasa za makundi ili kuweza kujenga chama imara na kama kuna changamoto zitatuliwe ndani ya chama kupitia vikao kwa kuwekana sana na baada ya kutoka tuwe kitu kimoja badala ya kuongelea sehemu zisizostahili," alisema Dk Mpango.

Alisema kama kuna tofauti na zimeshindikana ni bora kuwatumia wazee ndani ya chama ili kupata busara zao na kutatua changamoto zilizopo.

"Tiba ipatikane mapema na kuwe na mahusiano mazuri kati ya viongozi wa chama na serikali ili kuwaletea maendeleo wananchi ambapo mahusiano mabaya yanasababisha kuzoofisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ya elimu,afya,maji,barabara

## Kigoma yaanza kutolewa 'gizani'

Na Fadhili Abdallah, Kigoma

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande amesema ili kukabili upungufu wa umeme mkoani Kigoma, wameanza kufunga mashine mbili katika kituo cha kuzalisha umeme mjini Kigoma zitakazoongeza nishati hiyo kutoka megawati 6.2 za sasa hadi zaidi ya megawati 8.7.

Chande alisema hayo jana mjini hapa akiwa na Waziri wa Nishati, January Makamba ambako wamefika kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango alilotoa Septemba 22, mwaka huu kuwataka washughulikie tatizo hilo.

Chande alisema wakati hali ya ufungwaji wa mashine ukiwa hivyo tayari, Wilaya ya Buhigwe imeondolewa kupata umeme kutoka mashine za Kigoma na kurudishwa wilayani Kasulu, na kwamba hadi kufikia mwishoni mwa Novemba mashine mbili za kituo cha kuzalisha umeme mjini Kigoma kilichopo eneo la Bangwe zitakuwa zimeshafungwa.

Alisema hiyo ni mipang ya muda mfupi kwani mipango ya muda mrefu ni kukamilisha miradi ya umeme wa Gridi ya Taifa ambako awamu ya kwan ni umeme wa msongo w kilovoti 132 kutoka Tabo ambao utakamilika Okto mwakani, huku umeme kutoka Mto Rusumo mk Kagera kupitia Kakonko unatarajia kukamilila m 2023.

Sambamba na hilo, alisema upo mradi wa

Scanned with CamScanner




MAKAO MAKU

# Wafugaji watakiwa kutoa ushirikiano wakati wa sensa

Na Anastazia Anyimike

WAFUGAJI nchini wametakiwa kutoa ushirikiano kwa makarani wa sensa ili takwimu za mifugo zitakazopatikana zikaisaidie serikali kutatua changamoto zinazowakabili.

Mwito huo umetolewa na mwakilishi wa Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Dk Bedan Masuruli.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao kati ya viongozi wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Taasisi za Fedha na wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), kwa ajili ya kupokea muongozo wa utambuzi wa mifugo na ushiriki wa sensa ya watu na makazi ya 2022.

«Nitoe rai kwa wafugaji kutoa ushirikiano kwa wale watakaokuja kuhesabu sensa ili kuhakikisha kwa upande wa mifugo takwimu sahihi zinapatikana na zinakuwa wazi, ambazo zitaisaidia serikali kutatua changamoto zinazowakabili wafugaji hapa nchini,» alisema.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Anne Makinda, aliwahakikishia wafugaji kuwa serikali imeweka mazingira wezeshi kuhakikisha changamoto zilizojitokeza katika sensa ya mwaka 2012 zinatatuliwa ili zisijitokeze kwenye sensa ijayo.

Makinda alisema kufanyika kwa sensa ya mwaka huu kutaleta mapinduzi katika sekta ya mifugo kwa sababu itabaini idadi ya mifugo yote iliyopo Tanzania.

«Niwahakikishie kuwa serikali imeweka mazingira wezeshi na sensa ya mwaka huu itakuwa ya kipekee sana kwa sababu tumefanya maandalizi ya kutosha kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa.

«Lengo la kujua idadi ya mifugo litairahisishia serikali kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo na maeneo ya kunyweshea mifugo maji ili wafugaji wafuge kwa tija.»

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Jeremiah Wambura, alisema Chama kimepokea maelekezo ya serikali ya kufanyika kwa sensa na kuahidi kutoa ushirikiano ili azma ya serikali ifikiwe.

Akiwasilisha mada kuhusu Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, mtakwimu kutoka Ofisi ya Takwimu (NBS), Fausta Ndigiti, alisema moja ya aneo ambalo sensa italiangalia ni kutambua wafugaji kwa idadi na idadi ya mifugo.

# 'Cha gha

Na Sifa Lubasi

WATA takiw ya C punguza ghara kwa wanaopat virusi vya coro

Imeelezwa kw mmoja hutumia oksijeni kati ya 1 siku na gharama ni Sh 50,000, was 550,000 kwa siku



Mratibu wa Ujenzi Meshack Bandaw zote kujadili maen Maelezo).

# Wapew

Na Anastazia An Dodoma

KATIBU M ya Sanaa, na Michez Abassi, ametoa s machifu kuwasil ya kimila na kiut serikali iweze ku kuyafanyia kazi.

Dk Abassi aliya wakati wa kufung uliokutanisha mac kujadili mustakab utamaduni pamoj maoni ya kuboresh Utamaduni ya Mw

Alisema machi kuhakikisha wana na kuweka mipan iweze kutekelezw

«Hivyo muwe yale ambayo mna katika kuimarisha utamaduni wetu. tutayaweka kwen yako mengine aml

Scanned with CamScanner

kimkakati ikiwamo ya sekta ya kilimo.

Serikali imelinunua shamba hilo kutoka kwa Mfilisi, Silvanus Mlola,

wake kwa taifa.

Alisema uamuzi huo wa serikali umezingatia eneo hilo lilipo na malengo

kipindi cha makubaliano, hivyo kushindwa kufikia matarajio na makubaliano yaliyofanywa na serikali

serikali kwa ushirikiano na kukamilisha kwa wakati makubaliano yaliyofikiwa katika suala hilo.

HABARI LEO UK 8

# *TADB yataka ushirikiano sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi*

**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja kwa kuhimiza ushirikiano endelevu wa wateja wake na wadau mbalimbali katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kama njia ya kuhamasisha uwekezaji zaidi katika sekta hizo muhimu kwa uchumi wa taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema jana kuwa, benki hiyo imetumia Wiki ya Wateja kuhamasisha Watanzania hasa vijana kuchangamkia fursa kwenye sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

"Sisi kama TADB tunayo dhamana kubwa ya kuchagiza maendeleo na ukuaji wa sekta hizo ili ziweze kutoa mchango stahiki katika ukuaji wa uchumi wa taifa sambamba na kumwezesha mkulima, mfugaji na mvuvi kuongeza uzalishaji na kukuza kipato chake," alisema Nyabundege wakati akizungumza na wateja na wadau wengine wa benki hiyo mkoani Mbeya.

Alisema mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Songea, Songwe na Rukwa ipo katika nafasi nzuri ya kuzalisha mazao ya chakula na biashara na hivyo kuimarisha mnyororo wa thamani ya mazao nchini.

"Nimefurahi kuonana na kuwasikiliza wadau mbalimbali wa benki ambao wametoa ushuhuda wao namna benki hii ilivyowasaidia kuongeza uzalishaji na thamani ya bidhaa zao," alisema.

Wakati akiwa Nyanda za Juu Kusini, Nyabundege alizungumza na viongozi wa serikali za mikoa hiyo, wakulima na wafugaji ambao walionesha imani kwake na wakaomba ushirikiano wa benki hiyo na atembelee miradi iliyodhaminiwa nayo.

Alisema TADB ina jukumu la kutekeleza malengo ya serikali yaliyosababisha kuanzishwa kwake na kujipanga kuwafikia wakulima, wafugaji na wavuvi kwa wakati na ufanisi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Kampuni ya Forever Investment inayojihusisha na kilimo cha kahawa mkoani Songwe, Jane Daima, alisema benki hiyo imekuwa ni faraja kwa wakulima kwa kuonana nao kujadiliana mambo mbalimbali na uongozi wa juu.

"Hii ni nafasi pekee kwangu na wadau wengine wa kilimo kukutana na viongozi wa ngazi za juu wa benki hii na kufanya mazungumzo yenye tija katika kuboresha huduma hususani upatikanaji wa mikopo itakayosaidia kuboresha shughuli zetu za kilimo," alisema Daima.

Akilihutubia Bunge, Aprili mwaka huu baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita, Rais Samia Suluhu Hassan, alieleza umuhimu kuiongezea fedha TADB itoe mikopo mingi yenye riba nafuu kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao yatakayokuwa malighafi katika viwanda nchini.

Alisema serikali imedhamiria kuifanya Tanzania nchini ya viwanda ifikapo mwaka 2025 na sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zina nafasi kubwa katika kufanikisha azma hiyo.

Scanned with CamScanner

andani ya
kuhifadhi
mapato,"

atarajiwa
a Kwala

wa Mradi
SUMA JKT,
ati.

a Ujenzi,
ewa 44
hini, TRC
watakao
vizuri ili

reli ya kati
dombinu
Mbarawa.
chini ya
o na zile
kusanya

emu ya
ti ya Dar
enzi wa
ufufuaji
bahewa



**WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea taarifa ya Wilaya ya Kilwa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Zainab Kawawa, katika Ukumbi wa Kwa Sultan, mjini Masoko, mkoani Lindi, jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).**

UHURU UK 6

# Waziri Ndaki atatua kero ya wafanyabiashara wa dagaa

**Na SCOLASTICA MSEWA,** *Tunduma*

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka maofisa uvuvi kuacha kuwatoza ushuru wa kusafirishia mazao ya uvuvi nje ya nchi wafanyabiashara wa dagaa kwa lengo la soko la ndani ya nchi kwenye Mkoa wa Songwe.

Alitoa maagizo hayo jana wakati akiongea na wafanyabiashara wa dagaa katika mji wa Tunduma wilayani Momba, mkoani Songwe akiwa katika ziara yake ya siku mbili, ambapo wafanyabiashara hao walidai wamekuwa wakitozwa ushuru huo wakati baadhi yao hawasafirishi dagaa nje ya nchi.

Waziri Ndaki alisema wafanyabiashara wanaopaswa kutozwa ushuru wa usafirishaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi, ni wafanyabiashara wa dagaa ambao hununua na kuuza kwenye masoko yaliyopo nje ya Tanzania, ambapo kwa Tunduma huuzwa zaidi nchi za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Hivyo aliwataka maofisa uvuvi kuacha kuwatoza ushuru huo wafanyabiashara wanaouza dagaa kwenye soko la ndani.

"Tuache mara moja kuwatoza wafanyabiashara wa dagaa ambao wanauzia kwenye soko la ndani, ushuru wa kusafirishia mazao ya uvuvi nje ya nchi katika Mkoa wa Songwe kwa kigezo wote wanaziuza nje ya nchi," alisema Waziri Ndaki.

Aidha, Waziri Ndaki aliwataka wafanyabiashara hao kufanya biashara kwa kufuata taratibu zilizowekwa na kuacha tabia ya kutorosha dagaa kwa kutumia njia zisizo rasmi kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru.

Ndaki aliwaeleza kuwa endapo mfanyabiashara atakamatwa kwa kosa la utoroshaji dagaa, atanyang'anywa leseni, mzigo wa dagaa na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Awali, Mbunge wa Jimbo la Momba, Condester Sichalwe, akiongea kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo la Tunduma, Ernest Silinde, ambaye hakuwepo kwenye ziara hiyo, alisema suala la wafanyabiashara wa dagaa katika soko la ndani ya nchi kwenye Mkoa wa Songwe kutozwa ushuru wa usafirishaji mazao ya uvuvi nje ya nchini ni kero ya muda mrefu, ambayo imekuwa ikiwaumiza wafanyabiashara hao na wananchi wanaonunua dagaa.

Mfanyabiashara wa dagaa, Shaban Ally, alimshukuru Waziri kwa maamuzi aliyoyachukua ya kuondoa ushuru huo kwa wafanyabiashara wanaouza dagaa kwenye soko la ndani kwani kilikuwa ni kilio chao cha muda mrefu.

Scanned with CamScanner



jana. (Picha na MAELEZO).

# Wavuvi Tumbatu watakiwa kuacha uvuvi haramu

WAVUVI wa Kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, wametakiwa kutumia Hifadhi ya Uvuvi ya Kisiwa cha Tumbatu (TUMCA), kwa kulinda mazingira na kuachana na uvuvi haramu ambao umekuwa chanzo cha uharibifu wa mazalia ya samaki na matumbawe.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Makame Machano Haji, alitoa rai hiyo alipokutana na Kamati ya Uvuvi wa Hifadhi ya Kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja na wataalam kutoka Idara ya uvuvi kuhusu uvuvi unaozingatia mazingira jana.

Haji alisema serikali imeanzisha hifadhi ya uvuvi wa Kisiwa cha Tumbatu ili kulinda mazingira ya samaki, yakiwemo matumbawe ambayo yamekuwa yakihujumiwa kutokana na uvuvi haramu.

Aliwataka wavuvi wanaoendesha uvuvi katika maeneo hayo kuzingatia masharti ya uvuvi, yakiwemo kuacha kutumia nyavu zenye macho madogo ambazo ni hatari kwa mazalia ya samaki na matumbawe, na mazao ya baharini, kama vile mwani.

"Uvuvi haramu ukiwemo wa kutumia nyavu zenye macho madogo na wa kuzamia kwa kutumia bunduki haukubaliki hata kidogo...unatishia mustakabali wa rasilimali ya samaki na mazalia yake," alisema.

Mkuu wa Hifadhi ya Uvuvi ya Kisiwa cha Tumbatu (TUMCA), Said Shaib Said, alieleza kuwa athari za uvuvi haramu zimejitokeza katika maeneo ya hifadhi, hivyo baadhi ya samaki ambao ni maarufu kama pweza, ngisi na kamba hivi sasa wamekuwa adimu.

"Maeneo ya TUMCA tunakabiliwa na uhaba wa samaki ambao ni maarufu wanaopendwa kutumiwa na watalii wakiwemo pweza, ngisi na kamba kutokana na kasi ya uvuvi haramu wa kuvunja matumbawe," alisema.

Mvuvi maarufu katika kisiwa cha Tumbatu, Machano Haji ambaye awali alikuwa akijishughulisha na uvuvi wa kuzamia kwa kutumia bunduki, alieleza kuacha rasmi kuvua samaki kwa kutumia aina ya uvuvi huo, baada ya kubaini athari nyingi za kimazingira.

"Athari za uvuvi haramu tumeziona kwa wavuvi wa Kisiwa cha Tumbatu, ikiwemo kupungua kwa mapato yanayotokana na samaki kwasababu ya kupungua kwa samaki maarufu wenye fedha katika soko," alisema.

**UVUVI**

**UCHUMI**

Athari za uvuvi haramu tumeziona kwa wavuvi wa Kisiwa cha Tumbatu, ikiwemo kupungua kwa mapato yanayotokana na samaki kwasababu ya kupungua kwa samaki maarufu wenye fedha katika soko.



Joel Nanauka
SAIKOLOJIA

Maswali na majibu
Simu: 0756 094 875
email: joenauka@gmail.com

## Pigana bila kuchoka kufikia malengo yako ya maisha

Siku zote watu wenye nguvu zaidi sio wanaoonyesha uhodari wao hadharani bali wanaopigana vita ambavyo wengi hawavijui kabisa.

Ni rahisi kuwasifia watu wengine ambao unaona wamefanikiwa na kuna wakati unataka kuwa kama wao ila usichokijua ni kuwa kilichowafanya wawe hivyo ni ushindi juu ya vita ambayo wameendelea kupigana kila siku ambavyo wewe huvioni.

Usidanganyike na kufikiri unaowaona wamefanikiwa katika maeneo yao basi wamefika walipo kirahisi na kila kitu ni rahisi. Wapo ambao wakati wewe unaona wametulia na wameshafika, wenyewe wako kwenye vita vikali vinavyowakosesha usingizi.

Kwa kawaida mambo tunayoyajua kuhusu watu wengine ni machache ukilinganisha na ambayo hatuyajui kuhusu maisha yao. Hii inamaanisha unapotamani kuwa kama mtu fulani, kimyakimya unakuwa unatamani kupigana na kushinda vita ambavyo na yeye alivishinda pia.

Kuna wakati watu wanakusifia jinsi ulivyopendeza lakini moyoni mwako unajua vita unayopigana kuokoa ndoa yao. Wakati wengine wanasema ninyi ni ndoa ya mfano, wewe unajua namna unavyojitahidi kusahau mikasa iliyotokea kati yenu.

Kuna wengine wakikuona unatoka nyumbani kuelekea ofisini, wanatamani kazi uliyonayo bila kujua kuna wakati unatamani usiende ofisini kwa sababu bosi wako anakunyanyasa kila siku. Hawajui jinsi unavyopigwa vita na kufanyiwa hila ili kukuharibia, haya yote hawajui kabisa.

Wanapokuangalia kama kiongozi, wanatamani kuwa kama wewe ingawa wewe unatamani kuacha ili uwe mtu wa kawaida. Wakati wao wanasifia unavyopendwa na kukubalika, hawajui gharama ya kutolala unayoilipa, hawajui usivyopata muda wa kukaa na familia yako au maumivu ya kimyakimya unayovumilia ukiwa peke yako.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba vita unavyovishinda ukiwa peke yako ndiyo hukufanya uwe mtu wa maana mbele ya wengine. Kama kuna changamoto unakabiliana nayo kwenye biashara yako, uhusiano au ofisini, usikubali kukata tamaa.

Ili ufike upande wa pili ni lazima ushinde vita inayokukabili. Matajiri hawalali hivyo biashara yako haiwezi kusimama na ikawa ya mfano kama unapenda kulala. Jitume, usiku na mchana ukikumbuka kuwa vita vinavyokukabili huanzia katika akili yako.

Usikubali kuamini kuwa hautoweza kuinuka tena wala usiamini kuwa hakuna mlango mwingine wa kutokea baada ya ule wa mwanzo uliouzoea kufungwa.

### DONDOO

**Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi kubwa ya mifugo**



BIASHARA

## ‘EAC kuwe na cheti kimoja cha Uviko-19’



**Nairobi.** Wakurugenzi wa kampuni za sekta binafsi wameitaka Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuandaa utaratibu wa kutoa cheti kimoja kitakachotambulika katika nchi zote wanachama ili kuharakisha shughuli za biashara kukufua uchumi ulioathirika na janga la Uviko-19.Mapendekezo hayo yametolewa kwenye mkutano uliozikutanisha taasisi za sekta binafsi kutoka nchi wanachama na kufanyika jijini Nairobi, Kenya mapema wiki hii ukiratibiwa na Baraza la Biashara la Jumuiya hiyo (EABC).

Ofisa Mtendaji mkuu wa EABC, Dk John Kalisa amesema "vyeti vya chanjo ya Uviko-19 vitarahisisha utambuzi wa waliochanja hivyo kuondoa gharama za kutakiwa kupima tena kila unapovuka mpaka." Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Francis Nanai amesema Tanzania imeridhia Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) hivyo kufungua fursa nyingi.

# *Sababu bei vifaranga vya kuku kupaa zatajwa*

Aurea Simtowe, Mwananchi
asimtowe@mwananchi.co.tz

Miezi michache tu tangu kugundulika kwa janga la Ugonjwa wa Virusi vya Korona (Uviko-19) duniani, biashara ya mifugo nchini ilianza kuyumba kwani uingizaji wa mayai na vifaranga wa kuku wazazi ulioporomoka kuanzia Januari 2020.

Uviko-19 ni ugonjwa ulioanzia nchini China Novemba 2019 na kusambaa duniani kote na kuyaacha mataifa yakiathirika kiuchumi kutokana na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na maambukizi yake. Sasa hivi juhudi zimeelekezwa katika utoaji chanjo.

Kuchuka kwa uingizaji wa mayai na vifaranga wazazi nchini kumesababisha bei kupanda hivyo kuwaweka wafugaji katika wakati mgumu. Licha ya kupanda kwa bei, upatikanaji wake sio wa uhakika.

Mfugaji wa kuku eneo la Mbezi Msumi jijini Dar es Salaam, Obison Obadia anasema hata bei ya chakula nayo ipo juu jambo linalowapa wakati mgumu kufuga kwa tija waliyoizoea.

"Vifaranga vimeadimika sana, ukiweka oda ya leo unavipata baada ya miezi minne. Nadhani uzalishaji wa vifaranga umepungua nchini," anasema Obadia.

Kuadimika huko, anasema kumesababisha bei kupanda hadi Sh2,400 kutoka kati ya Sh1,500 hadi Sh1,800 ya zamani.

Bei hiyo haijapanda Dar es Salaam pekee kwani Irmelgard Sangana, mfugaji wa wilayani Mufindi anasema hali imekuwa ngumu kwani mfugaji anapokosa vifaranga maana yake hafanyi chochote.

"Bei ya ya vifaranga imepanda na ya chakula pia lakini ile tunayouza kwa wateja wetu bado iko vilevile. Serikali iweke mazingira rafiki kuongeza uzalishaji wa vifaranga nchini pamoja na mayai ya wazazi," anasema Irmelgard.

Kuhusu kutumia mashine za kutotoleshea mayai kukabili uhaba uliopo, Irmelgard anasema ni ngumu kwani kutakuwa na uwezekano mkubwa wa kuzalisha kuku wanaotoka kwenye ukoaa mmoja jambo ambalo sio zuri kwa ufanisi wa mfugaji.

"Kuku wazuri hawatakiwi kutoka ukoo mmoja kwani kuna uwezekano mkubwa wa kupata magonjwa yanayofanana. Hili likitokea, utapata hasara ya matibabu au kuchelewa kukua. Viwandani wanatumia teknolojia ya kisasa kutokana na ukubwa wa mtaji walionao," anasema.



Kuhakikisha Watanzania hawakosi kitoweo cha kuku wakitakacho, Serikali iliruhusu uingizaji wa mifugo hiyo na kati ya Juni na Agosti, mayai 874,000 na vifaranga wazazi 905,000 waliingizwa nchini kutoka Kenya, Malawi, Uganda, Afrika Kusini na Uturuki ili kupungufu pengo lililopo. **Picha Maktaba**

### TAKWIMU

**80m**

**Wastani wa idadi ya kuku waliopo nchini wengi wakiwa wa kienyeji wanaofugwa kibiashara ingawa maeneo mengi kuna kuku wa kienyeji.**



### Wazalishaji na mawakala

Mwananchi lilitembelea kiwanda cha Interchick kuangalia uwezekano wa kupata vifaranga baada ya kupata majibu yasiyoridhisha kutoka kwa mawakala.

"Bei ya kifaranga ni Sh1,700 lakini kwa sasa hatupokei oda mpaka baadaye ndiyo tutafungua. Oda zitakazotolewa Oktoba ni kwa ajili ya mwakani," alisema muhudumu aliyekutwa mapokezi akiwahudumia wateja ingawa hakuwa na uhakika oda hizo zitaanza kupokelewa tarehe gani.

Gazeti hili pia lilienda ofisi za kampuni ya Ikhlas inayozalisha vifaranga lilikoambiwa wamesitisha kutotolesha vifaranga wa kuku wa nyama.

"Tuna kama miezi miwili hivi hatuzalishi kwa sababu upatikanaji wa mayai umekuwa wa shida. Mwanzo tulikuwa tunanunua mayai lakini kwa sababu hayapatikani tunaona bora tununue kuku wazazi kutoka nje ya nchi ili tuwe tunapata mayai yetu wenyewe," alisema Khamis Mgendwa, ni mmoja wa wamiliki wa kiwanda hicho.

Kuadimika kwa mayai hayo, anasema kumewalazimu kupandisha bei ya vifaranga hadi Sh2,500 kwa kila kimoja lakini wanaendelea kupokea oda nyingi wanazoshindwa kuzitekeleza.

Changamoto iliyopo kwenye viwanda vinavyozalisha vifaranga inaenda mpaka kwa mawakala ambao wanalazimika kukataa fedha za wateja wanaowapokea kila siku.

Anne Msumba, wakala anayepatikana eneo la Tazara jijini Dar es Salaam anasema "hata sisi tunatamani hizo oda lakini vifaranga hakuna. Mfugaji asipopata vifaranga maana yake wakala haingizi kamisheni."

Wakala mwingine aliyejitambulisha kwa jina moja la Yusuph alipoulizwa uwezekano wa kupata vifaranga alisema "ndani ya wiki hii nitakudanganya, maana oda ni nyingi na vifaranga wanaokuja ni wachache. Bei ni Sh2,400."

Wakati wafugaji wakiathirika zaidi kutokana na uhaba uliopo, baadhi ya mawakala wasio waaminifu wamepata upenyo wa kujipatia kipato kisicho halali kwa kuwauzia wakulima vifaranga vya majogoo ambavyo huchelewa kukua hivyo kutumia chakula kingi kuliko kawaida.

"Vijogoo (male chicks) ukuaji wake sio wiki nne kama kuku wa nyama makoo. Vifaranga hivi vinauzwa na mawakala wa mitaani sio kutoka kwenye kampuni moja kwa moja," anasema Anold Sawe, mfugaji wa Mbweni jijini hapa.

### Kupanda kwa chakula

Bei ya chakula nayo imepanda kutoka wastani wa Sh62,000 kwa mfuko wa kilo 50 hadi Sh68,000.

Katibu wa Chama cha Wafuga Kuku Kibiashara Tanzania, Thabiti Batenga anasema janga la korona lilisababisha mashamba mengi ya kuku wazazi duniani kufungwa huku akitumaini hali kukaa sawa kuanzia Januari mwakani.

"Jambo hilo lilisababisha upungufu wa vifaranga kwa asilimia 30. Usafirishaji wa kuku na mayai kuja Afrika ulipungua sana," anasema Batenga.

Kuhusu chakula anasema bei ya mashudu ya soya ambayo huchukua asilimia 35 ya chakula cha mifugo imepanda kutoka Sh1,200 hadi Sh2,400. "Sisi soya tunaagiza kutoka nje na bei yake ilianza kuongezeka miezi mitano nyuma," anasema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Kuku wa Nyama Dar es Salaam, Gloria Michael anasema uhaba ulianza tangu Desemba 2020, kila aliyetoa oda alitakiwa kusubiri kati ya miezi mitatu hadi minne hali inayowaumiza zaidi wafugaji wadogo kwa sababu kipaumbele huelekezwa kwa wakubwa.

"Mfugaji mdogo ukimwambia asubiri miezi mitatu kupata vifaranga na hana kazi nyingine anayotegemea zaidi ya hiyo atapata wapi fedha za kujikimu?" anahoji Gloria.

Kudhibiti uhaba unaojitokeza nchini, mwenyekiti huyo anashauri kuanzishwa kwa mamlaka itakayosimamia uzalishaji na kuzuia kupandishwa kwa bei kiholela kuanzia vifaranga, mayai mpaka chakula.

"Starter sasa hivi inauzwa hadi Sh78,000 na kifaranga unakipata hadi kwa Sh2,600. Ukienda Interchick kiwandani, kifaranga ni Sh1,900 lakini kwingine Sh2300, kungekuwa na mamlaka inayosimamia bei ingedibitiwa," anasema Gloria.

Zuwena Almasi, analia na bei anayouza vifaranga wachache aliowapata na gharama alizoingia kuwakuza akisema "safari hii bila Sh6,500 siuzi, bora nile mwenyewe. Sitacheka na mlanguzi."

> **Baada ya kuona uhitaji bado ni mkubwa, wizara imeruhusu tena uingizaji kwa kuanzia Septemba hadi Novemba ili kupunguza uhaba huu**
>
> Profesa Hezron Nonga, mkurugenzi wa huduma za mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.



Vifaranga vya kuku ambavyo kwa sasa vimepanda bei hivyo, kuwafanya wafugaji wadogo kufikiria kupandisha bei ya kuku.

### Serikali yafafanua

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga anasema Serikali inatambua uhaba uliopo ambao ulianza tangu Januari mwaka jana na ilishafanya utafiti kujua ukubwa wa tatizo.

Baada ya kulifahamu, anasema Serikali iliruhusu kuingiza vifaranga kutoka nje kwa miezi mitatu kuanzia Juni hadi Agosti na tathmini inaonyesha kampuni 13 ziliingiza mayai 874,000 na vifaranga 905,000 ambacho bado ni kiasi kidogo.

"Baada ya kuona uhitaji bado ni mkubwa karibu, asilimia 70, wizara imeruhusu tena uingizaji kwa kuanzia Septemba hadi Novemba ili kupunguza uhaba huu," anasema Profesa Nonga.

Uchunguzi uliofanywa na wizara, mkurugenzi huyo anasema ulibaini vituo 15 vilivyopo vinaweza kutotolesha mayai 2,168,200 kwa wiki hali inayowafanya wafugaji kusubiri kwa kati ya wiki tatu mpaka sita baada ya kutoa oda ndipo wapate mzigo.

"Uviko-19 ndio umefanya upatikanaji wa vifaranga kuwa wa tabu sana, bei navo imeongezeka, kifaranga wa kuku wa nyama anafika hadi Sh2,800 kitu ambacho si cha kawaida, kifaranga wa kuku wa mayai anauzwa hadi Sh4,000 na unatakiwa kusubiri," anasema Profesa Nonga.

Kwa hatua zinazoendelea kuchukuliwa, anasema itachukua muda kidogo kurudi kwenye hali ya kawaida kwani baadhi ya mashamba ya yameanza kuingiza kuku wazazi na ya nje yanafunguliwa.



WATAALAMU

## Marekani yaisaidia Zanzibar kukabili Uviko-19



**Unguja.** Serikali ya Marekani imeajiri wataalamu 100 watakaosaidia kutoa elimu na chanjo ya Uviko-19 visiwani Zanzibar. Wataalamu hao wameajiriwa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia mradi wa afya endelevu. Mkurugenzi wa Afya wa USAID, Ananthy Thambinayagam amesema nguvukazi na vifaa vya kutosha ni muhimu kwa maendeleo endelevu na utoaji endelevu wa huduma za afya na mwitikio dharura kipindi hiki cha janga la Uviko-19. "USAID inasaidia upatikanaji wa wataalamu kwa sababu nguvukazi yenye uwezo inaokoa maisha hasa katika janga la Uviko-19," amesema Ananthy.

Wataalamu hao watafanya kazi katika vituo vya afya 33 maeneo manne ya bandari yanayotumiwa kuingilia visiwani humo. Katika utekelezaji wa majukumu yao, wataalamu hao wanatarajiwa kuharakisha kasi ya utoaji chanjo kote, Unguja na Pemba. Msaada huo unalenga kusaidia upatikanaji na utoaji wa chanjo, kupunguza magonjwa na vifo vitokanavyo na korona.

### Kingo
By James Gayo



Scanned with CamScanner

:aifa
gazi
amu
wa
nwi-

Ofisi
nge,
enye
a ali-
i wa
nzuri
a na
slahi

tafiti
wa
wan-
sisha
ra ili
ya
izazi
kana

ekiti
kim-
atma
nka-
ume

# Vijana watakiwa kuchangamkia fursa za kilimo, uvuvi na mifugo

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Mbeya.** Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) imeadhimisha wiki ya wateja kwa kuhamasisha Watanzania hususani vijana kuchangamkia fursa lukuki zilizopo kwenye sekta za kilimo,mifugo na uvuvi.

Akizungumza na wateja pamoja na wadau wengine wa benki hiyo mkoani Mbeya, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege alisema wanahimiza ushirikiano endelevu wa wateja wake pamoja na wadau mbalimbali katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kama njia ya kuhamasisha uwekezaji zaidi katika sekta hizo muhimu kwa uchumi wa Taifa.

"Tunayo dhamana kubwa ya kuchagiza maendeleo na ukuaji wa sekta hizo ili ziweze kutoa mchango stahiki katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, sambamba na kumwezesha mkulima,mfugaji na mvuvi kuongeza uzalishaji na kukuza kipato chake," alisema Nyabundege.

Nyabundege alisema Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Songea, Songwe na Rukwa ipo katika nafasi nzuri ya kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara na hivyo kuimarisha mnyororo wa thamani ya mazao hapa nchini.

Nyabundege akiwa nyanda za juu kusini alifanya mazungumzo na viongozi mbalimbali wa Serikali za mikoa hiyo, wakulima na wafugaji ambao walionyesha imani kubwa kwake na kumuomba kuwaunga mkono sambamba na kutembelea miradi iliyodhaminiwa na benki hiyo.

"Nimefarijika kujionea mwenyewe nini kinachofanyika na kusikiliza changamoto za wakulima na kuwa an uelewa mpana wa namna ya kukabiliana nazo," alisema Nyabundege.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Kampuni ya Forever Investment inayojihusisha na kilimo cha kahawa mkoani Songwe, Jane Daima aliishukuru benki kwa kumwalika kwenye maadhimisho ya wiki ya wateja ambapo imekuwa ni faraja kuonana na kujadiliana mambo mbalimbali na uongozi wa juu wa benki ya TADB.

"Kwa kweli nimefarijika sana na nimejifunza vitu vingi kuhusu benki hii na uwekezaji katika kilimo, mifugo na uvuvi,"alisema.

Scanned with CamScanner

# Govt sets aside 50bn/- for Kilwa modern fish port

From DEOGRATIUS KAMAGI in Kilwa

THE government has set aside 50bn/- to be spent on construction of a modern fishing port in Kilwa District, Lindi region, as part of efforts to promote the fishing sector in the country.

Prime Minister Kassim Majaliwa made the statement yesterday here, saying the project is part of government's effort to promote fishing sector and in turn, raise living standards of people in the region.

He said upon completion, the state-of-art port will handle and oversee the management of the country's coastal and marine resources and modernise fishing industry in the Southern Zone.

"President Samia Suluhu Hassan has dedicated her efforts in serving Tanzanians ... she has approved a total of 50bn/- to be used in the construction of this fishing port in Kilwa district. This is big project that will improve lives," added the Premier.

He further said the scheme has been endorsed by the Ministry of Fisheries and Livestock Development, Ministry of Works and Transport, as well as the Tanzania Ports Authority (TPA).

Mr Majaliwa, who is in Lindi region for a five day work visit, also asked residents of Kilwa District to make better use of the upcoming project, by developing business plots to guarantee accommodations of facilities and people upon its completion.

"Those who have secured land within the district should start developing it, because upon completion of the port project... visitors who will be coming here, will need accommodation in terms of hotels and other facilities," he suggested.

Upon completion, the project will also play a crucial role in increasing revenue collections for Kilwa, whose current annual collections stands at an average of 5bn/-.

In a related development, Mr Majaliwa asked officials in Kilwa District to be creative and utilize the available opportunities in raising revenue collections in the area.

He said, as the central government keeps on allocating the budget for development projects in the Local Government Authorities (LGAs), it's crucial for them to come up with efforts aimed at raising their revenues.

"There are a lot of opportunities which are yet to be utilized here, you have to be creative and make better use of all the resources available," he pointed out. In another development, the Prime Minister suspended three revenue collections officers in Kilwa District over involvement in the loss of revenues in the council.

Suspended officials are Mr Bahaye Shilungushela, Mohamed Samadu and Ally Kin'yonge.

"Kilwa is a giant council in terms of revenue collections, the government will never tolerate any form of theft... we shall continue taking strong measures against those who will temper with public funds," he said.

Earlier, the Lindi Region Commissioner Zainab Telack briefed the Premier that they have been improving in revenue collections, adding, "Improving revenue collections in all councils within the region has been among my top priorities, we shall continue working on it."



## Security firm hosts HIV self-testing campaign

By DAILY NEWS Reporter

SGA Security hosted the launch of the HIV-self-testing at workplace aimed at creating awareness for employees to use the kits to know their sero-status.

Making the revelation while delivering the kit, the Association of Tanzania Employers (ATE) representative Hellen Mkwizu, said the move was aimed at ensuring that employees know their sero-status and hence take initiative to take care of their health.

She further said the initiative was driven by their association in partnership with PSI Tanzania, TACAIDS and the Ministry of Health.

Scanned with CamScanner